

***Mpendwa Rafiki,***

Tunatumai kuwa wote mnaafya njema na shughuli zinakuendea vizuri, wewe pamoja na rafiki zako. Kama mliyoy wengi wenu nasi pia ni waislamu na tunatumaini kuwa Mwezi wa Ramadhani ulikuwa ni wakati mzuri kwa kila mmoja.

Kama ilivyo kwa mwezi Septemba kila mwaka, tungependa tena kuzungumzia kuhusu siku ya kimataifa ya kuushinda umaskini ambayo wengi wetu huisherehekea katika tarehe 17 Oktoba, siku ambayo iko karibu sana kutoka sasa.

Hata hivyo, mara zote tumekuwa tukianza na kijarida hiki kikiwa na shuhuda ya kujitoka. Mara hii, tumechagua shuhuda ambayo itatambulisha pendekezo letu kwa sherehe za Oktoba 17 za mwaka huu.

***Dear friend,***

We hope everything is fine with you, your relatives and your friends and that you are all in good health. As many of you and us are Muslim, we also hope that Ramadan was a nice time for everybody.

As every year in September, we would like to speak again about the World Day to Overcome Extreme Poverty when we will be many celebrating on October 17<sup>th</sup>. This day is coming very soon.

However, as you know we always start this Newsletter with a testimony of commitment. This time we chose a testimony to introduce our proposition for how we can celebrate October 17<sup>th</sup> this year.

**Harakati za kijamii huko Bangui**

*“Kokoro Boeing ni kitongoji maskini sana huko Bangui (Jamhuri ya Afrika ya Kati) : hakuna maji safi ya kunywa, umeme, barabara nzuri za magari, na kadhalika. Kuanzia mwezi Mei kila mwaka, msimu wa mvua unapoanza, mara zote kitongoji hicho hukumbwa na mafuriko na baadhi ya nyumba hubomoka. Ushahidi huu unaendelea husababisha mwendelezo wa uwepo wa mbu na hatimae ugonjwa wa malaria.*

*Baada ya kampeni ya kukuza uwelewa juu ya afya, baadhi ya akinamama wa kitongoji hicho walipata wazo la kusafisha mitaro na waliwahamasisha waume zao na vijana wao wa kiume. Kila mmoja alitakiwa kutoa mchango wake wa fedha au vifaa ili kusaidia shughuli hiyo. Shughuli hii ilifanikiwa kwa sababu watu tofauti tofauti walikubali kuja pamoja : wazazi, vijana na hata halmashauri na viongozi wa kitongoji ambao waliutia moyo mradi huo. Kazi hii kwa pamoja ilileta maendeleo kwa afya za familia zote na kugusa kila mmoja.*

*Usafi wa kilometa za mtaro ulizuia mafuriko*

**Community action in Bangui...**

*“Kokoro Boeing in Bangui (RCA) is a very poor neighbourhood : no drinking water, no electricity, no suitable ways for vehicles... Every year from May, when the raining season comes back, the neighbourhood is regularly flooded and some houses collapse. This permanent wetness causes the development of the mosquitoes and of malaria.*

*After a campaign raising awareness for health, some mamas of the neighbourhood had the idea of cleaning the draining channels and they mobilised their husbands and their sons. Everybody was invited to bring his or her contribution, through money or tools, in order to support the work. This work was a success because very different people agreed to come together : parents, young people and even the City and neighbourhood leaders who encouraged this project. This work together brought improvement for health of all the families and concerned everybody.*



ATD Fourth World Movement - P.O. Box 61786 - Dar es Salaam  
mail : [atd.tanzania@gmail.com](mailto:atd.tanzania@gmail.com)

English website : [www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html](http://www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html)

Tovuti ya Kiswahili : [www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html](http://www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html)

ambayo yangetokea hapo baadaye. Ilihataji muda mrefu sana kuanza mradi lakini sasa inaonyesha uzoefu mzuri kuhusu kinachowezekana kupitia umoja wao.”

Itakuwa haina maana kuuhukumu ushuhuda huu uliotajiri na wenye kuvutia. Inatuonyesha ni jinsi gani shughuli za kijamii zinavyoweza kufanikiwa kama hali za kimsingi zinajitosheleza.

*The cleaning of several kilometres of channels avoided future floods. It needed a long time for starting the project, but it represents now a positive experience about what is possible through the unity of everybody.”*

This testimony speaks for itself, it is impressive and meaningful. It shows us how a community workshop can be a success if the basic conditions are satisfied.



## Kuelekea Oktoba 17

Kama ambavyo tayari mnafahamu, siku ya kimataifa ya kuutokomeza umaskini uliokithiri husherehekewa kila mwaka duniani kote na taasisi mbalimbali, jumuiya, serikali, jamii mbalimbali, na kadhalika. Siku hii ni fursa ya kuwaunganisha watu wasiojiweza pamoja na wale ambao wako tayari kuungana nao katika jitihada zao.

Ni muhimu kuwasaidia watu maskini sana kuwa ni sehemu muhimu kabisa katika siku hiyo, kuwaruhusu kusema na kusikika, kuhusu ari yao ya kujituma na matendo yao katika kubadili maisha ya baadaye ya watoto wao. Kwa kweli, siku hii inaweza kusherehekewa mahala popote kama unapoishi, mahala pakazi, msikitini au kanisani kwenu, na kadhalika. Sherehe hizi mara kadhaa zimekuwa si za majisifu, huandaliwa na vitendea kazi vichache : Hii ni njia ya kuonyesha kuwa kuushinda umaskini uliokithiri pia ni suala la kujitoa binafsi na si suala la fedha. Baadaye, msisite kukusanyika watu wachache hata kwa kusoma sentensi ambazo ni kiini cha siku hii.

**“Popote pale wanaume na wanawake wanapohukumiwa kuishi katika umaskini uliokithiri haki za binadamu zimevurugwa.**

**Kuungana pamoja ili kuhakikisha kwamba hizi haki zinaheshimiwa ni jukumu letu sote.”**

Joseph Wresinski

## Towards October 17<sup>th</sup>

As you already know the World Day to Overcome Extreme Poverty is celebrated every year throughout the world by many institutions, associations, governments, communities, etc. This day is an opportunity to gather the most disadvantaged people who fight every day and those who are ready to join them in their struggle. It is essential to help the very poor people to be really at the centre of this day, allowing them to speak out and to be heard, about their initiatives and actions to change the future of their children. Of course this day can be celebrated in any place you are living, your working place, your mosque, your church... The celebrations are often simple and organised with very few means : it is a way of showing that the overcoming of extreme poverty is also a question of personal commitment and not only a question of money. Consequently don't hesitate to gather a few people even just to read the sentence which is at the origin of this day :

**“Wherever men and women are condemned to live in extreme poverty, human rights are violated.**

**To come together to ensure that these rights be respected is our solemn duty.”**

Joseph Wresinski



## Shughuli za kijamii

Kwa mwaka wa pili hapa Tanzania, jumuiya ndogo ndizo zinazohusika kujadili, kuandaa na kuitangaza Oktoba 17 nchini. Mwaka huu, kundi hili liliamua kuongeza njia mpya ya kuisimika siku hii katika taratibu za kawaida za kusherehekea : katika maeneo yetu mbalimbali, tunatakiwa kufanya "shughuli ya kijamii". Hii ni kuhusu nini ?

Katika sehemu ya kwanza ya kijarida hiki, tulikuwa na mfano nzuri wa shughuli za kijamii.

### **Kuwa na kila mmoja...**

Shughuli ya kijamii inamaanisha kuwa, ni kazi ambayo wanajamii wanaalikwa kuishiriki : haimaanishi kuwa ni wale wenye ujuzi tu, wanajamii wote inamaanisha hata wale ambao hutengwa pia, watu walio na ulemavu, wale ambao hawatambuliwi na jamii kama ni sehemu ya jamii na kadhalika. Si rahisi kufanya hivi...

Wakati mwingine miradi ya kijamii inapoanza, watu maskini huwa hawaji, hawashiriki. Wao ndio pengine wanaohusika lakini wanafikiri kuwa : *"Sina wazo lolote la kutoa, wengine wananikejeli, kunikosa"*. Siku moja mzazi wa kiume alimwambia mmoja wetu :

*"Huwa sijihusishi na kazi kama hizi, hakuna anayekuja nyumbani kwangu ili kuomba msaada wangu. Ndio maana sishiriki"*.

Japokuwa sisi sote tuna dhamira kuwa dunia yenye usawa inawezekana, dunia ambayo hakuna atakaekwa anatengwa, tunajuwa kuwa ni ngumu kutambua hata kwa kiwango kidogo, hata hivyo inawezekana. Inahitaji muda kujongea na kumuelezea kila mtu kuwa uwepo wake ni muhimu na baadhi ya mambo yanawezekana kufanywa au kusemwa na yeye tu kisha kidogo kidogo watu ambao hawahisi kuhusika wanaweza kuanza kuja na kushiriki. Inahitaji pia kukaa nao, kuunga mkono mapendekezo yao, kufanya kazi pamoja, kujaribu kuwapendekeza wao kushika majukumu. Na kazi inapokwisha, ni muhimu kugusia kwa uchache mchango wa kila mtu... Si rahisi sana lakini inawezekana kabisa.

## A community workshop.

For the 2<sup>nd</sup> year in Tanzania, a small group of associations is in charge to think about, prepare and promote October 17<sup>th</sup> in the country. This year this group decided to add a new way of marking the day to our usual way of celebrating : in our different places, we are invited to organise a "community workshop". What does this mean ?

In the testimony of this Newsletter, we had a good example of a community workshop.

### **With everybody...**

A community workshop means a day in which all the members of the community are invited to participate : all the members means not only the most dynamic and the most skilled, all the members means also those usually excluded, the handicapped people, those who are not recognised by the community as being part of it... This is not easy to do...

Sometimes when a community project starts, the poorest people don't come, don't participate. They are probably the most concerned, but they think, *"I don't have any idea to give, the others are going to make fun of me, to criticise me"*. One day a father told one of us, *"I'm never associated to this kind of work. Nobody comes up to my home in order to ask me for my help. That is why I don't participate"*.

Even though all of us have the conviction that a fairer world is possible, a world in which nobody would be excluded, we know that it is tough to realise even on a small scale... However it is possible. It takes time to explain to everybody that his or her presence is important, that some things can only be done or said by him or her... Time is needed to meet people especially the most excluded, and explain why their participation is essential. Then little by little people who did not feel concerned start to come and participate. We must pay special attention to the most disadvantaged, ensuring their participation, remaining close to them, supporting their propositions, working together, suggesting them to take responsibilities. And when the work is over, it is important to highlight the contribution of everybody... Not so easy but very possible !



## Kwa heshima ya utu wetu ulio sawa.

Sisi sote ni tofauti sana, baadhi yetu ni imara na wengine ni dhaifu, baadhi ni wazuri katika kazi za mikono na wengine kwa hadithia hadithi mbalimbali... Lakini sisi ni sawa mbele ya haki za binadamu ambazo zinatakiwa kuheshimiwa kwa kila mtu, pia sisi sote ni sawa katika utu kwa sababu pekee ya kuwa ni wanaume na wanawake bila kujali uwezo na ujuzi wowote tulionao, japokuwa tumekuwa tukiharibiwa na maisha yaliyo magumu sana.

Mwanamama anayefanya kazi katika zahanati pembeni ya mji wa Ouagadougou (Burkina Faso) alisema : *"Tunapokuwa mbele ya mtu, kwanza tunatakiwa kufahamu kuwa yeye ni mwanadamu. Kitu muhimu ni heshima kwa utu. Haina maana kumpa mtu kitu ikiwa utamfedhehesha kwa kufanya hivyo."*

Kivipi tunayoyafanya yanairuhusu jamii kutambua usawa wa kiutu kwa walio maskini kabisa miongoni mwao.

## **Kipaumbele kwa watu walio wekwa kando zaidi**

Katika hali fulani, shughuli za kijamii zilikuwa zikipagwa ili kuleta faida kwa wadau wote wa jamii. Hata hivyo, watu wengi sana wanakubali kuhamasishana ili kusaidia shughuli hizo : kwa mfano kusaidia majirani zao ambao wako katika hali ngumu : *"Ni kawaida kuwapa kipaumbele wote walio maskini sana. Tulifanya hivyo pale ambapo ukuta wa nyumba ya jirani yetu ulipobomoka baada ya mvua kubwa sana kunyesha. Tumewaomba marafiki wanaoishi katika eneo hilo na kushirikiana katika shughuli hiyo tukiwa na ari ya kusaidiana. Ukuta ulijengwa upya kwa haraka na kila mmoja alikuwa na furaha sana, yaani wale wanaoishi katika nyumba hiyo na washiriki wote katika ujenzi wa ukuta wa nyumba hiyo."*

Sherehe za siku ya kimataifa ya kupambana na umaskini uliokithiri zitakuwaje mahali penu ? Njia tofauti tofauti za kusherehekea zinawezekana na kile kitakachofanywa na kila mmoja wetu kitategemeana na nyenzo alizo nazo vitu muhimu kuliko vyote ni kuwahusisha wasiojiweza kabisa katika jamii ili kutambua ushiriki wao.

Tuambie umepanga kufanya nini au ulifanya nini!

*Wako, Timu ya ATD Dunia ya Nne  
ya Dar es salaam.*

## In the respect of our equal dignity...

All of us are very different, some are strong and others are weaker, some are good at doing manual work and others at telling stories... But we are equal in the face of human rights which have to be respected for everybody. We are equal in dignity, because we are women and men, whatever our abilities and skills are, even for those of us who have been damaged by a hard life.

A lady working in a dispensary in a suburb of Ouagadougou (Burkina Faso) said : *"When we are in front of a person, first we have to discover the human being. The most important is the respect of the human dignity. It is not useful to give somebody something if you are humiliating him or her by doing that"*.

Whatever we are doing, does it allow the community to recognise the equal dignity of the poorest of its members ?

## **The priority to the most abandoned people...**

In some cases, a community workshop is organised to bring a benefit to all the members of the community. However, many people accept to mobilise themselves in order to support, for example their neighbours who are in great difficulties. *"It is normal to give priority to the poorest. We did it when the wall of our neighbours' house collapsed after very big rains. We asked friends, people living in the same area and we shared the work with the spirit to help one another. The wall was very quickly rebuilt and everybody was very happy, both the people living in the house and all the participants in the rebuilding."*

How will the celebration of the World Day to Overcome Extreme Poverty be this year in your place ? Very different ways are possible and what will be done by everybody of us will be depending on his or her means. The most important is to associate the most disadvantaged in our communities in order to recognise their involvement.

Tell us about what you plan to do or what you did !

*Your ATD Fourth World Team  
in Dar es Salaam*